

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA
Simu Na: +255 26 2321607
Nukushi: +255 26 2322116
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:-



*Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.*

TANGAZO LA KUITWA KAZINI

Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inapenda kuwataarifu waombaji kazi wa nafasi mbalimbali za kada za afya waliowasilisha maombi katika kipindi cha mwezi wa April, 2023 kuwa mchakato wa kuwapangia vituo vya kazi umekamilika kwa awamu ya nne. Awamu hii ni kwa ajili ya kujaza nafasi wazi **42** za Watumishi ambao hawakuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa awamu ya Pili katika kipindi cha mwezi **Septemba 2023**.

Mwezi Aprili, 2023, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilipata kibali cha ajira ya watumishi **8,070** wa Kada mbalimbali za Afya. Baada ya mchakato wa ajira kukamilika, jumla ya waombaji wa ajira wenye sifa wa kada za afya **7219** walipangiwa vituo vya kazi.

Waombaji wote walio pata nafasi wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo: -

- a) Kuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Aidha, waombaji watakaoshindwa kuripoti kwenye vituo vya kazi ndani ya siku kumi na nne (14) nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine haraka iwezekanavyo.
- b) Kuwasilisha Vyeti Halisi (**Original Certificates**) vya Kidato cha Nne, Sita, Chuo Kikuu, NACTE na vyeti halisi vya usajili wa mabaraza ya kitaaluma kwa ajili ya kuhakikiwa na mwajiri kabla ya kupewa barua ya ajira.

- c) Waombaji waliopata nafasi za ajira watakaoripoti bila ya kuwa na Vyeti Halisi (**Original Certificates**) vya Kidato cha Nne, Kidato Sita, Chuo Kikuu, NACTE na vyeti halisi vya usajili wa mabaraza ya kitaaluma hawatapokelewa.
- d) Waombaji waliopata nafasi za ajira wanajulishwa kuwa hakutakuwa na nafasi ya kubadilisha vituo vya kazi walivyopangiwa.

Waombaji wote ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili, watambue kuwa hawakupata nafasi hivyo wasisite kuomba kwa mara nyingine nafasi za kazi zitakapotangazwa.

Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kuwapokea, kuhakiki vyeti na kuwafanyia mafunzo elekezi (Induction Course) kabla ya kuwapangia vituo vya kazi.

Orodha ya majina ya waombaji waliopangiwa vituo vya kazi inapatikana kupitia tovuti ya OR-TAMISEMI www.tamisemi.go.tz

Limetolewa na:

Katibu Mkuu,

Ofisi ya Rais - TAMISEMI,

Mji wa Serikali – Mtumba,

S.L.P. 1923,

DODOMA.

26 Januari, 2024